BARTIMAYO KIPOFU

. . .?. . .jalia Roho Wako Mtakatifu aliye mkuu, Bwana, aje usiku wa leo katika nguvu na kufanya miujiza mikubwa miongoni mwetu, akiwaponya wagonjwa, akiwaita nyumbani kwenye Kimbilio katika wakati wa dhoruba, wale waliochoka barabarani. Jalia wale ambao wamepotea njia iliyoandaliwa, warudi usiku wa leo, na wapatanishwe na Mungu. Tujalie, Bwana.

2 Na tutakapoondoka usiku wa leo, tunaomba ya kwamba Wewe utafanya jambo fulani miongoni mwetu, ambalo litakuwa la ajabu sana hata litatufanya twende nyumbani mwetu tukisema kama wale waliokuwa wakija kutoka Emau, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?" Kwa kuwa tunaomba, katika Jina Lake na kwa ajili Yake. Amina.

3 Mwaweza kuketi. (Asante, Ndugu Roy.) Sisi ni . . . Barua hizi, tunaziombea. Tunathamini imani yenu katika maombi yetu. Baadhi yazo zimepigwa muhuri, zingine, zinaletwa ma—mahali ninapokaa, hazina, stempu, kwa hiyo tunazirudisha moja kwa moja upesi tu tuwezavyo.

4 Tulikuwa na usiku mzuri sana, jana usiku, sivyo? Roho Mtakatifu alitubariki.

5 Sasa, ninaona chini kwenye—kwenye ukumbi wa wapiga muziki hapa, watu kwenye machela na vitanda vya wagonjwa. Sasa, kusudia tu niani mwako sasa, ya kwamba huu ndio usiku wa mwisho utakaoteseka, utaenda nyumbani usiku wa leo uwe mzima. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Utaamini tu hilo moyoni mwako, hutavunjika moyo. Kwa kawaida, tunapokea kile tunachotarajia kuona, kile tu tunachotarajia.

6 Kama ningeweza kushuka kwenye ukumbi huo mdogo, na kuwatoa ninyi watu mle, na kuwapa afya, ningefanya hivyo. Ningefurahi sana kufanya hivyo, bali siwezi kulifanya, mimi ni mwanadamu tu, kama mtu huyu hapa. Na la—laiti ningaliweza. Lakini ninajua ya kwamba Bwana wetu yupo hapa, Naye Ndiye anayeweza kuwafanya mtoke kwenye hizo machela, mwende nyumbani na muwe wazima. Ninatumaini ya kwamba Yeye atafanya hivyo, si hilo tu, bali ninyi nyote kote kwenye kusanyiko.

7 Vema sana kuona kusanyiko hili zuri usiku wa leo, umati mzuri wa watu. Basi ndugu yetu wa thamani tayari amenena Neno, nami ninataka tu kuchukua dakika chache sasa, kwa kuwa kila usiku, sijaribu kuhubiri usiku, ni kufanya tu mchezo mdogo wa kuigiza, mpaka nipate hisia ya wasikilizaji. Nina hakika mnaelewa ninalomaanisha.

8 Ndipo basi, Bwana akipenda, ninataka kuhubiri Jumapili alasiri juu ya somo: *Mfano Wa Tai Ataharikishavyo Kiota Chake Na Kupapatika Juu ya Makinda Wake*, yaani, Bwana akiruhusu, Jumapili alasiri.

9 Sasa usiku wa leo, mpaka tu—mpaka kwa namna fulani tutakapofahamiana, na . . . Yote haya ni ya kiroho, ninawaangalia kama wanadamu, kama nilivyo mimi mwenyewe, lakini kila mmoja wenu ana roho. Ndipo basi wakati upako wa Roho Mtakatifu unapokuja, karibu ni kama pumzi, ndipo unaweza kuhisi imani, kutokuamini, na chochote kile.

Sasa, unasema, "Hiyo ni saikolojia, Ndugu Branham."

10 Labda ndivyo ilivyo, kama ndivyo ilivyo, Bwana wetu aliitumia, kwa sababu Yeye—Yeye alimtoa mtu mmoja nje ya mji wakati mmoja kumwombea. Halafu wakati mwingine, tunajua ya kwamba kulikuwa na msichana aliyekufa nyumbani, nao watu walikuwa wakifanya maombolezo makuu juu yake. Naye akawatoa hao watu nje, akawaacha tu wazazi wake, na Petro, Yakobo, na Yohana, na Yeye Mwenyewe, ndipo akamfufua huyo msichana katika wafu. Mnaona, kuna jambo fulani kulihusu.

11 Na kila mmoja, unaangalia, jicho lako ndilo lango la nafsi yako, unaweza kukiangalia, karibu linatawala zile hisi zingine. Unakiangalia kabla ya kukionja, unakiangalia kabla ya kukinusa, na kukigusa, na kadhalika, kwa kawaida jicho ndilo lango la nafsi. Basi unapoangalia, na laiti ungaliweza tu kuacha hilo liwe baraka kwako! Unapoona kwa macho yako mwenyewe, usikie kwa masikio yako mwenyewe, Bwana Yesu akitenda kazi miongoni mwa watu na kufanya mambo ambayo amekuwa akifanya, inapaswa kukufanya uwe na imani halisi.

12 Sasa, hutamwona katika mwili wa kawaida, mpaka atakapokuja kwa ajili yako kwenye ule ufufuo mkuu, wa kiama, ndipo tutamwona. Ndipo tutajua jinsi tunavyojulikana, tutamwona jinsi alivyo. Hiyo ndiyo saa ambayo sisi sote tunaitamani, tukiingojea, wakati huo. Hadi wakati huo, Roho Wake yupo hapa, nalo Kanisa linazidi kuwa kama Yeye wakati wote.

13 Tangu yale matengenezo makubwa ya kwanza katika Luther, Kanisa lilikuwa na mpanuko mkubwa, ambao ulikuwa bado ni Roho Mtakatifu akitenda kazi katika siku za Luther; ndipo likaingia katika uchache tena wakati John Wesley, utakaso, kazi ya pili ya neema, ndivyo alivyoiita; ndipo basi, moja kwa moja ikaja Pentekoste, kule kurudishwa kwa vipawa, likaendelea kupungua; na linazidi kupungua sasa mpaka Kanisa na Kristo watakuwa Mmoja. Itakapotukia, Kuja kwa Bwana kutatimia, na ufufuo wa wote waliolala katika Yeye utatukia: Walutheri, Wamethodisti, Baptisti, Presbiteri, wote walio na Roho Wake, watafufuka kukutana na Yeye hewani. Mungu, jalia wakati huo mara moja. "Hata hivyo, njoo, Bwana Yesu."

14 Nilikuwa . . . Liko niani mwangu, lazima niliseme. Nilikuwa na kisa cha jambo hilo, hapa, wakati fulani uliopita, ambapo nilienda kwenye m—mji fulani, tulikuwa tukifanya mkutano, na mahali fulani huko Ohio, siwezi kukumbuka mahali hapo sasa hivi, basi kulikuwa na mkutano mkubwa, kiasi kwamba, nilitoka nikaenda barani kukaa katika moteli ndogo. Kulikuwa na mkahawa mdogo wa Dunkard kando ya barabara. Maskini wanawake wazuri kuliko wote, safi kuliko wote walifanya kazi mle ndani, walioonekana sana kama Wakristo.

15 Nami nilikuwa nimefunga kwa yapata siku tatu. Nao hao ndugu wakaendelea na ibada. Nilipaswa kuhubiri Jumapili hiyo alasiri, sikuwa naenda kuwa na ibada ya uponyaji, nami kidogo nilikuwa na njaa, kwa hiyo nikawaza, "Nitaenda kwenye mkahawa huo mdogo." Lakini walikuwa wamefunga, wameenda kanisani, ilikuwa Jumapili. Basi ng'ambo tu ya barabara, kituo cha mafuta, na maskini mkahawa mdogo wa kawaida wa Kimarekani, kama pale, duka dogo la sambusa.

16 Hili linachukiza kulazimika kusema jambo hili, bali ni kweli. Basi nilipoingia, kulikuwa na polisi amesimama, yapata umri wangu, hakika ameoa, naye alikuwa amemkumbatia mwanamke fulani, akicheza mashine ya kuchezea karata. Kamari ni haramu huko Ohio, na hapo alikuwa akicheza kamari, nikawaza, "Vema, sheria!"

17 Nikaangalia upande wa nyuma, na baadhi ya hao wavulana, kama wahuni wakiwa na hizo nywele ndefu shingoni mwao, na—na jaketi za ovaroli, na, loo, na wamezivuta chini, mwajua, nguo chini kwenye nyonga zao, alikuwa amesimama pale amemkumbatia kwa mkono mhudumu wa kike mwenye umri wa miaka kumi na sita, mahali hawakupaswa kuwa nayo. Nikawaza, "Loo, rehema!"

18 Kisha nikaangalia mkono wangu wa kulia, kulikuwa na mwanamume, wakati wa kiangazi, amevaa koti kubwa refu, koti la serikali, skafu kubwa ya kijivu shingoni mwake, mwanamume mwingine ameketi karibu naye, pamoja na mwa—mwanamke mkongwe, mwenye umri wa kutosha kuwa nyanya yangu. Naye alikuwa amejipaka rangi hii ya makucha usoni mwake, chochote mnachokiita kitu hicho, maskini ninii nyeusi . . . Mimi hutamka hilo vibaya kila wakati. Mnaiitaje hiyo? Ni kitu fulani . . . kwa namna fulani . . .

19 Nawaambia, si ya Wakristo, hilo ni jambo moja la hakika. Mimi ni mmishenari, hiyo ni tabia ya kikafiri. Hiyo ni kweli kabisa. Wapentekoste walikuwa hawafanyi hivyo, lakini sijui kilichotukia. Walikuwa hawakati nywele zao, lakini si—sijui kilichotukia, mtu fulani alilegeza kamba, mahali fulani. Tulizoea kuukariri wimbo mdogo, maskini mhubiri wa Kimethodisti alizoea kuimba:

Tulilegeza kamba, tulilegeza kamba,

Tulipatana na dhambi.
Tulilegeza kamba, kondoo wakatoka nje,
Lakini mbuzi waliingiaje?

20 Jibu: Mlilegeza kamba.

21 Maskini bikizee, nywele zilizoonekana za samawati, alikuwa ameketi hapo, amevaa maskini nguo ndogo, fupi, ambazo mtu angeona aibu kuvaa, naye ameketi hapo, na alikuwa amelewa. Ndipo nikaangalia kote, nikawaza, "Loo, rehema!" Nikawazia, "Mungu, ninii Wako anawezaje. . .? Unawezaje Wewe, ukiwa mtakatifu na mwenye haki, hata kuangalia kitu kama hicho? Inaonekana kana kwamba ungekiondolea mbali kitu hicho. Je, inambidi maskini Sarah na Rebekah wangu kulelewa, mahali kama hapo?"

22 Ndipo hao watu wawili wakaomba radhi, na kuondoka, walisema wangerudi katika dakika chache. Nami nilikuwa nimesimama pale nikimtazama yule mwanamke, nikimkosoa kwa yote kwa uwezo wangu wote, huku nikiwazia, "Ni jambo la kuchukiza jinsi gani!"

23 Lakini mara nyingi, hatupaswi kufanya hivyo, hatujui ni nini hadithi ya ndani. Basi ikawa kwamba, Mungu alinifundisha somo papo hapo.

24 Nikarudi tu nyuma ya mlango, Kitu fulani kikasema, "Rudi nyuma." Ndipo wakati ni—nilipopiga magoti kuomba, niliangalia nikaona ono la ulimwengu ukigeuka namna *hii*, ulionekana kama umezungukwa na mnyunyizo wa rangi nyekundu. Nami nikajiona, kama ilivyokuwa kwanza, nimesimama duniani, na kila wakati ningefanya kosa, dhambi zangu zingeelekea kwa Mungu, lakini Yesu alitenda kama bamba la kunizuia, dhambi zangu zisimfikie Mungu.

25 Na kila wakati ningefanya kosa, basi ilionekana kana kwamba dhambi zangu zingeelekea kwa Mungu, na ndipo Yesu angezidaka, nami ningeona machozi yakitiririka mashavuni Mwake, na Damu ikitiririka usoni Mwake, Naye angeangalia juu, na kusema, "Baba, hajui afanyalo, msamehe," namna hiyo.

Nikawaza, "Je, hizo ni dhambi zangu zinazofanya hivyo?"

26 Nami nikaenda karibu Naye, nikaangalia, na kulikuwa na kitabu kilichokuwa kimefunguliwa, nazo dhambi zangu zilikuwa mbaya sana juu yake. Ndipo nikasema, "Mpendwa Bwana Yesu, unamaanisha ya kwamba dhambi zangu ndizo zilizoumiza ubavu Wako, na kusababisha machozi machoni Pako, na—na Damu usoni Mwako?"

Akasema, "Naam."

Nikasema, "Naomba unisamehe."

Naye akagusa ubavuni Mwake, akaandika kwenye kitabu, "Amesamehewa," akakitupa nyuma Yake.

Nikasema, "Loo, daima nitakushukuru Wewe."

27 Basi alipofanya hivyo, akasema, "Ninakusamehe, lakini unataka kumhukumu." Ndipo alipofanya hivyo, nilikuwa nikimtazama yule mwanamke tena.

28 Nikaenda mahali alipokuwa, nikasema, "Hujambo?"

29 Alikuwa akinywa pombe kupita kiasi, nami nikasema... Akaniangalia na kusema, "Loo, u hali gani?"

Nami nikasema, "Naweza kuketi chini?"

Akasema, "Nina wenzangu."

30 Nami nikasema, "Si hivyo. Ninataka tu kukwambia jambo fulani." Nami nikaketi chini na kumwambia. Nami nikamwangalia, naye alikuwa akilia, ndipo nikasema, "Hivi huoni aibu?"

Akasema, "U nani wewe? Wewe ni mhudumu huyu hapa chini kwenye ghala la silaha?"

Nikasema, "Naam, mama, Ndugu Branham."

31 Akasema, "Ninaona aibu kukukabili, Ndugu Branham." Akasema, "Baba yangu alikuwa mhudumu wa Kimethodisti. Nina binti wawili, mmoja wao ni Mkristo mashuhuri sana, huyo mwingine ni mwalimu wa shule ya Jumapili." Naye akanisimulia hadithi ya mume mlevi, na kile alichoanzisha. Akasema, "Hakuna matumaini kwangu."

32 Nikasema, "Kama hakuna matumaini kwako, kwa nini Mungu akanionyesha ono hilo?" Na hapo, nikamshika mkono, nikapiga magoti pale kando ya kibanda kile, na kumwongoza kwa Bwana Yesu, moja kwa moja kwenye chumba hicho.

33 Nilipoamka, yule polisi alikuwa amesimama pale, msichana huyo alikuwa amesimama pale nyuma, akilia, na ikaleta tofauti. Mnaona, hatuna budi kuyaangalia mambo jinsi yalivyo, mnaona, hatujui kilicho nyuma ya hiyo hadithi.

34 Hebu na tufungue sasa katika Luka Mtakatifu, mlango wa 18, kifungu cha 38. Ningetaka kusoma hili kwa ajili ya mazungumzo mafupi tu kabla hatujaomba, na kuwa na...kwa ajili ya wagonjwa.

> *Akapiga kelele akisema, Yesu, Mwana wa Daudi, unirehemu.*

35 Mandhari yetu inafunguka kwenye lango la kaskazini la mji wa Yeriko, mnamo mwaka wa A.D. 33. Hapana shaka ilikuwa ni asubuhi yenye baridi, alikuwa amechelewa, alikuwa akiota usiku kucha, kwamba angeweza kuona. Basi akaamka kwa kuchelewa, akashika njia kwenda kwenye maskini kituo chake ama mahali alipoombea. Na loo, katika siku hiyo kulikuwa na ombaomba wengi. Kama hawakufika malangoni mapema, wakati watu walipokuwa wakiingia kwenye biashara zao

mjini, mbona, iliwabidi kumshika huyo mtu. Labda wangeweza kumudu sarafu moja kwa siku kwa ombaomba mmoja.

36 Lakini sasa ilionekana wote walikuwa wameingia, na hapo akaachwa peke yake. Asingeweza kumsikia mtu yeyote barabarani. Aliangalia, ninamaanisha, alisikiliza asikie mtu akija, hakuna mtu aliyekuwa anakuja. Kwa hiyo anaenda kule na kujitwalia jiwe, na kuketi chini. Ndipo akaanza kuwazia juu ya usiku alipokuwa akiota. Ndipo akakumbuka. . .

37 Jua hilo lenye joto la Kipalestina likaanza kumtia joto kidogo katika koti lake lililochakaa, alipokuwa ameketi juu ya jiwe hili karibu na ukuta, nje tu ya kivuli. Nao uso wake wenye makunyanzi ulikuwa umeelekezwa ardhini.

38 Na huenda alikuwa akiwazia jambo kama hili: Akili yake ikarudi nyuma kwa miaka mingi, kwenye ubavu uo huo wa kilima, ama karibu na Yeriko akiwa mvulana mdogo, wakati angeweza kuona, na jinsi alivyokuwa anapenda kukimbia huku na huku kilimani na kuchuma maua madogo ya kombe-tindi mwanzoni mwa majira ya kuchipua, na kulala chini ubavuni mwa kilima na kutazama mawingu meupe yakipita huku anga za samawati zikiakisi. Ulikuwa ni ulimwengu mzuri jinsi gani!

39 Na sasa yeye ni mzee, na kila kitu kimetoweka, naye ni kipofu, na anaomba riziki yake, jinsi ilivyoonekana maumbile yalikuwa katili kwake. Basi wakati alipokuwa akiwazia jambo hilo, alikumbuka jinsi ambavyo mama yake alikuwa akimwita kutoka upande wa pili wa kilima. Hapa yapata saa nane alasiri, alimwita ndani, na baada ya kula chakula chake cha mchana, angeninii. . .angeketi kwenye ukumbi wa kando ulioelekea mto Yordani, naye angemshika mikononi mwake, naye angepapasa nyuma maskini nywele zake nyeusi za Kiyahudi, zenye mawimbi, na—na kumbusu, na kusema, “Bartimayo, wewe ndiye mvulana mdogo mzuri kuliko wote ulimwenguni. Nina furaha sana kwamba wewe ni mvulana wangu mdogo.”

40 Na jinsi angeangalia na kuona mashavu yake mazuri, na macho makubwa, ya hudhurungi wakati yangetabasamu kwake, huku akimkumbatia mvulana wake mdogo mashavuni mwake na kumbusu. Na—naye alikuwa anapenda kumsikia akisimulia hadithi kabla hajampembeza alale.

41 Moja ya hadithi zake alizozipenda sana ilikuwa kuhusu mvulana mdogo. Wakati mmoja katika wakati wa Biblia. . . Angemwambia hadithi ya nabii mashuhuri mwenye nguvu aliyeishi, jina lake Elisha, aliyevaa joho la Eliya, akiwa na sehemu maradufu ya Roho yake. Na jinsi ambavyo mtu huyu alikuwa mtumishi mkuu wa Mungu, jinsi Mungu alivyoyaheshimu maombi yake, na kuwaheshimu wale waliomheshimu.

42 Naye alipitia katika mji fulani, na kulikuwako na mwanamke katika mji huu ambaye alikuwa ni mwanamke

mashuhuri, si Mwebrania, bali alikuwa Mshunami, bali alimheshimu mtu huyo kwa sababu alikuwa mtu mashuhuri wa Mungu, naye alimwamini Mungu. Na jinsi angemwambia juu ya heshima, yule mwanamke mashuhuri angemwomba aketi na kula pamoja naye na mumewe.

43 Siku moja alimwambia mumewe, "Ninaona ya kwamba mtu huyu anayekula pamoja nasi anapopita, akienda kwenye pango lake mlimani kwenye Mlima Karmeli kuomba, ninaona ya kwamba yeye ni mcha Mungu, mtu mtakatifu, mtu mashuhuri wa Mungu. Nafikiri tunapaswa kumfanyia jambo fulani." Nao wangeninii. . . Kasema, "Nakuomba, kando ya nyumba yetu hapa, hebu tumjengee nyumba yake ndogo tu, ili kwamba. . . Anaona aibu, labda, kuingia na kula pamoja nasi wakati wote, kwa hiyo hebu tumwekee tu meza ndogo huko nje, na beseni dogo la kufulia, na kinara kidogo cha taa, na kitanda, kiti anachoweza kupumzikia, naye anaweza kujiburudisha wakati akipita."

44 Basi wakati huyo nabii mkuu alipokuja na kuona hii, iliibariki tu nafsi yake kuona kwamba huyo mwanamke alimpenda Mungu vya kutosha kumheshimu mtumishi Wake. Basi huyo mwanamke. . . Basi nabii akamwambia mtumishi wake, Gehazi, "Nenda, umwulize kama ningeweza kuzungumza na amiri mkuu wa jeshi, ama fadhili fulani ambayo ningemtendea."

45 Ndipo huyo mtumishi akarudi, na kusema, "La, anasema anakaa miongoni mwa watu wake mwenyewe, wala hana haja ya kitu, 'Asante, hata hivyo.'" "Lakini," Gehazi akasema, "mume wake ni mzee, nao hawana watoto."

46 Kwa hiyo hapana shaka Mungu alimpa nabii ono. Ndipo aliposema, "Mwite mlangoni," basi aliposimama mlangoni, maskini yule nabii mzee, akasimama, na kusema, "BWANA ASEMA HIVI, katika wakati huu mwakani, utazaa mwana." Hata hivyo, huyo mwanamke asingeweza kuona jinsi hilo lingewezekana, lakini katika wakati uliowekwa alikuwa na mvulana mzuri, mdogo. Na jinsi alivyompenda mvulana huyu mdogo!

47 Nami ninaweza kumsikia akisema, "Bartimayo, unajua, wavulana na wasichana wadogo ni baraka za Mungu kwa familia. Ni kitu fulani kulihusu kinachoiunganisha familia pamoja. Unaona, Bartimayo, Mungu alimpa mwanamke huyo mpweke mvulana mdogo. Na Mungu alinipa mimi na mume wangu, baba yako, wewe, Bartimayo. Na sasa, wewe ni maskini hazina yetu hapa nyumbani. Loo, tunakupenda sana!" Naye angeweka mikono yake midogo shingoni mwake na kumkumbatia.

48 Huyo hapo sasa, mwenye makunyanzi na mzee, alikuwa ameondoka kwa miaka mingi.

49 Ndipo angesimulia hadithi jinsi huyo mvulana mdogo alivyotaka kumfuata baba yake, kasema, “Kama vile tu wewe, Bartimayo. Kuenda huko kondeni, ndipo siku moja, hapana shaka ilikuwa yapata wakati wa adhuhuri,” adhuhuri kuu huko Palestina. “Na hapana shaka jua lilimpiga, maana alipiga mayowe, ‘Kichwa changu, kichwa changu!’

50 “Baba yake alimrudisha nyumbani. Naye akaketi pajani mwa mama yake mpaka yapata wakati wa adhuhuri naye akafa. Lakini jinsi Mungu alivyohusika na mwanamke huyo! Jinsi alivyomchukua akaenda mahali pale padogo na kumlaza kitandani ambapo nabii alikuwa amelala, Mwakilishi wa Mungu, akimlaza kitandani. Akatandika nyumbu akaenda Mlima Karmeli.

51 “Huyo nabii hakujua shida yake ilikuwa ni nini, alimtuma Gehazi, na kusema, ‘Nenda, uone shida ya yule Mshunami, ana huzuni moyoni mwake, naye Mungu amenificha mimi.’”

52 Mungu hawaambii manabii Wake kila kitu. Yeye huwaambia watumishi Wake yale tu anayotaka wajue, si kitu kingine. Mnaona? Hawawezi kumfanya Mungu awaambie lolote, Mungu husema tu yale anayotaka kusema.

53 “Halafu, jinsi ambavyo yule—yule mtumishi aliichukua fimbo ya Eliya kwenda kuiweka juu ya huyo mtoto mchanga, lakini huyo mwanamke alishikilia. Alijua ya kwamba Mungu alikuwa ndani ya nabii huyo, naye akasema, ‘Sitakuacha.’ Alitaka kujua ni kwa nini Mungu alimpa huyo mtoto mchanga kisha akamchukua. Lakini unaona, mambo yote hufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wale wampendao Bwana.” Angemfundisha Bartimayo masomo hayo.

54 Halafu angesimama, na kusema, “Ingewezaje kuwa ni kwa wema kwangu kwamba mimi ni kipofu, basi? Lakini Mama, hapana shaka, alisema kweli.”

55 Kisha akaendelea na ndoto yake. Na baada ya kitambo kidogo, akaanza kuwazia tena, “Sasa, unajua Elisha aliingia kwenye chumba kile, akatembea huku na huku, huku na huku sakafuni, akaenda akaulaza mwili wake juu ya maskini mtoto huyo aliyekufa naye huyo mtoto akapiga chafya mara saba akafufuka.”

56 Loo, jinsi macho yake madogo yangeangaza, aseme, “Mama, Mungu huyo angali hai?”

57 “Loo naam, Mpenzi, Yeye anaishi mumu humu katika vilima hivi vya Uyahudi. Yeye hukaa moja kwa moja karibu na watu Wake, kamwe hawaachi.”

58 Hilo lilikuwa likipiga kengele moyoni mwake. Usiku kucha alikuwa ameota juu ya kuwa anaona tena. Akawazia, “Loo, jinsi lingekuwa ni jambo tukufu hapa, kama ningeweza kuona majani ya vuli yakianguka, kama mara nyingine

tena ningeweza kuangalia huku na huku." Upofu ni kitu cha kuchukiza sana, ulimwengu mzima umefungwa kwako, ulimwengu unaoonekana.

59 Na pale, ameketi pale, halafu basi alizoea kuwazia hadithi nyingine kuu, mama yake alikuwa ameketi barazani, ameangalia Yordani, naye angesema, "Bartimayo, moja kwa moja pale chini, chini ya nusu maili, chini tu ya kile kivuko, katika mwezi wa Aprili wakati theluji yote ilikuwa imeyeyuka na mto ulikuwa juu sana hapa bo—bondeni, Mungu aliwaongoza watu Wake upande ule mwingine, na kisha akafungua njia, wakavuka Yordani katika nchi kavu."

60 Naye angewazia juu ya hadithi hizo, angesema, "Loo, lakini ole, sijui kilichompata huyo Mungu mkuu. Kasisi wetu hutwambia ya kwamba siku za miujiza zimepita, mambo hayo hayawezi kutukia tena."

61 Hiyo ndiyo shida siku hizi, tuna msemo huo kwa wingi sana ya kwamba "Mungu alikuwako, bali hayuko sasa."

62 Biblia ilisema ni yeye yule jana, leo, na hata milele, ni Mungu tu siku hizi kadiri alivyokuwa wakati huo, na Yeye daima atakuwa Mungu. Kama aliwahi kuwa Mungu, Yeye daima atakuwa Mungu. Hawezi kufa, Yeye—Yeye hawezi kuzeeka, hawezi kubadilisha nia Yake, hawezi kufanya maamuzi mapya juu ya mambo ambayo tayari amefanya maamuzi juu yake. Uamuzi Wake wa kwanza ulikuwa sahihi na hauna budi kuwa sahihi milele, la sivyo alifanya uamuzi mbaya alipoufanya. Mnaona? Yeye hana budi kudumu na uamuzi Wake wa kwanza, Yeye ni mkamilifu, hana kikomo, wala hawezi kubadilika. Loo, hiyo ndiyo faraja ambayo hatuna budi kuwa nayo, mtu yeyote anayemtafuta Mungu hana budi kuwa na faraja hiyo imara kwamba Mungu hawezi kubadilika.

63 Ninaweza kusema jambo fulani, niseme samahani nililisema, huenda nilikosea. Lakini Yeye hawezi kusema hivyo, kwa sababu Yeye ni mkamilifu, Yeye hana kikomo. Sisi tuna kikomo, tunaweza kufanya kosa lolote lile, bali Yeye hawezi.

64 Na kama Yeye aliwahi kuitwa jukwaani kumponya mtu, Naye akamponya mtu huyo kulingana na imani yao, wakati mwingine anapoitwa, hana budi kumponya huyo mwingine, na huyo mwingine, na kila apataye kumjia. Kama akiitwa jukwaani kumwokoa mtu, Naye amwokoe kwa imani yake, kila aitaye kwa imani, hana budi kumwokoa. Hiyo ni kweli.

65 Pia kumbukeni, Mungu anapokuita, umebarikiwa unapojisikia Mungu anaita, maana "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipoitwa na Baba Yangu kwanza." Ni Mungu akibisha mlangoni mwa moyo wako. Vipi kama kamwe hakubisha? Wazia hilo. Hilo lingekuwa ni jambo la kuchukiza jinsi gani! Lakini Mungu humpa kila mtu nafasi, wewe mwenyewe unaikataa.

66 Wakati Bartimayo alipokuwa ameketi pale, mara akasikia kwato za maskini nyumbu zikishukia kwenye hayo mawe ya barabarni, zikishuka kutoka upande wa Yerusalemu. "Loo," anawazia, "huyu hapana shaka ni ta—tajiri anayekuja." Karibu njia pekee ya kusafiri wakati huo, ilikuwa ni kwa miguu ama kwa punda. Na—nao matajiri wangeweza kumpanda nyumbu. Huenda alisema, "Hapa hapana shaka ni mahali ninapoweza kupata sadaka."

67 Kwa hiyo anarudisha mikono yake nyuma, akikimbia kuelekea barabarani, ama, kuelekea barabara kuu, akisema, "Mnirehemu, mimi ni kipofu. Nililala kupita kiasi asubuhi ya leo, sina hata sarafu. Kuni zangu za majira ya baridi hazijaokotwa, hakuna unga kwenye pipa. Mwaweza kunisaidia tafadhali?"

68 Ndipo mtumishi anamsimamisha maskini huyo nyumbu, naye anasikia sa—sauti kali ikisema, "Simile, ombaomba! Mimi ni mtumishi wa Bwana, mimi ni kuhani kutoka Yerusalemu. Kutakuwa na mlokole, *anayejiita* nabii hapa leo hii, kufanya ibada ya uponyaji. Simile! Tutalichukua shirika la wahudumu huku chini na kuhakikisha hakuna kitu kama hicho kinachotukia jijini mwetu. Hatutaki yoyote ya hayo huku chini, hatuna mambo kama hayo huku chini."

"Ati nini?"

"Simile, ombaomba, sina budi kushika njia." Ndipo maskini yule nyumbu akasonga mbele.

69 Bartimayo akarudi. Sasa, jua lilikuwa limechomoza juu sana na kivuli cha ukuta kilikuwa kimerudi nyuma kidogo, kwa hiyo akajipatia jiwe karibu na lango, akipapasa hayo mawe ya kale ambapo kuta zilikuwa zimeangukia, naye akaketi juu ya jiwe hili. Ndipo akawaza, "Nilikuwa nikiota kuhusu nini? Ujana wangu, nilipokuwa ninaweza kuona, nilipokuwa mvulana mdogo. Nilikuwa nikiwazia juu ya Yehova Mungu mkuu, ambaye wakati mmoja alikuwako. Loo, hakika, mtumishi wa Mungu asingetenda hivyo. Ni kitu gani hicho alichoniambia kuhusu Nabii? Loo, nadhani sikulipata." Na kwenye . . .

70 Akaketi chini, akawaza, "Vema, unakumbuka, miaka mingi iliyopita, mama yangu aliniambia mara nyingi, kwamba moja kwa moja kwenye barabara ile ile, juu ya mawe yale yale walikuja Eliya na Elisha, wameshikana mikono, wakienda kuifungua Yordani."

71 Moja kwa moja juu ya mawe yale yale, si yadi ishirini kutoka mahali alipokuwa ameketi, siku moja, manabii wawili mashuhuri walitembea wameshikana mikono wakienda Yordani, barabara ile ile, mawe yale yale.

72 "Loo, laiti ningaliishi wakati huo, ningekimbia huko nje, na kusema, 'Watumishi wakuu wa Bwana Mungu, mwombeni tu Mungu, Mungu atayasikia maombi yenu, macho yangu

yatafunguka.'" Kama yule mvulana mdogo aliyesimama hapa jana usiku, aliyezaliwa kipofu. "'Macho yangu yatafunguka, nami nitaweza kuona, nami ninaweza kufanya kazi, na—na kupata riziki, na kadhalika. Kama . . .'

73 "Lakini ole, hao manabii wamekwisha, wanasema hakuna manabii tena, wala hakuna kitu kingine kilichosalia, naye Yehova ametuacha, wala hakuna tena . . . Siku za miujiza zimepita. Naye anatutarajia tu kuishi kwa ajili ya Mbingu juu, halafu basi tutakapokufa, tutaenda Huko juu, bali hakuna msaada kwetu, tena.

74 "Nami ninaamini, kama ningalienda huko nje kwa Elisha na Eliya, nisingalitendewa na hao watumishi wa Bwana kama nilivyotendewa na huyu, ambaye amepita hivi punde tu. Ninaamini wangalizingatia kisa changu, na angalau waniombee wakati wakipita."

75 Mnajua, kama mtumishi wa Mungu, unapaswa kuangalia kile unachofanya, kwa sababu ninyi ni nyaraka zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote. Ninyi Wakristo, sikuzote iweni tayari kusaidia, ama kufanya jambo fulani kumsaidia mtu, kufanya maisha kuwa rahisi na matamu zaidi kidogo kwao wanaponinii . . .

76 Unasema, "Vema, si—sina karama yoyote ya uponyaji."

77 Haikubidi kuwa nayo, angalau toa kitu fulani, omba dua, fanya jambo fulani. Wafanye wajisikie . . . Wafanyie vizuri zaidi uwezavyo, kwa vyovyote vile. Kamwe usimdharau, usimwonyeshe mtu yeyote madharau, haidhuru ni nini, hata kama wamekutesa, fanya hivyo, kwa vyovyote vile. Kama huwezi kufanya hivyo kutoka moyoni mwako, basi unapaswa kuja madhabahuni na kukaa mpaka roho huyo aingie ndani yako, ili kwamba kutoka moyoni mwako, unaweza kuwapenda wale wasiokupenda. Hapo ndipo Mungu atakapojibu maombi yako, kwa kuwa maadamu kuna chochote moyoni mwako, "Nikiwaza uovu moyoni mwangu, basi Mungu hatanisikia." Hivyo ndivyo Daudi alivyosema, na hiyo—hiyo ni kweli, Yeye hatakusikia.

78 Basi, Eliya alikuwa amepitia pale, na Elisha, wakishuka kwenda, bali maskini huyo kipofu alikuwa amefundishwa kwamba siku za miujiza zilikuwa zimepita.

79 Ndipo akakumbuka baada ya Yoshua kuvuka Yordani, kwamba yapata yadi mia tano kutoka mahali alipokuwa ameketi, Israeli walipiga kambi, wakapiga kambi yao. Ndipo siku moja, huyo shujaa mkuu, mwenye nguvu, Yoshua, aliyepachukua mahali pa Musa kuwaongoza hao wana kwenda katika nchi ya ahadi, basi wakati alipokuwa huko nje siku moja, akitembea huku na huku, akiangalia kuta za Yeriko, ambalo lilikuwa ndilo kusudi lake la kwanza kuuteka mji huo, wote walikuwa ndani, milango imefungwa, na mawe yao makubwa yamening'inizwa juu kuwarushia watakapokuja, naye alikuwa

akishangaa jinsi ambavyo angeweza kuuteka mji huo, kwa sababu walipewa huo, na jinsi Mungu alivyokuwa amepanga kufanya jambo hilo, ndipo ilitokea aliangalia, amesimama mbele yake, hapo alisimama Shujaa mwenye nguvu amechomoa upanga Wake. Ndipo Yoshua akauchomoa upanga wake, akatoka kwenda kumkabili, akasema, "Je, Wewe uko upande wetu? Je, uko upande wa adui zetu?"

80 Ndipo upanga ukametameta juu ya kichwa Chake, akasema, "La, Mimi ni Amiri wa jeshi la Bwana."

81 Huyo Yoshua mwenye nguvu akatupa upanga wake chini, akaitoa ngao yake, akaiweka chini, chapeo yake, akapiga magoti mbele Zake.

82 Ndipo kipofu Bartimayo akawaza, "Unajua nini? Hilo lilitukia papa hapa nje, huyo Amiri mkuu wa Jeshi la Bwana alikuwa amesimama ardhini, moja kwa moja huko nje, bali siku za miujiza zimepita." Hakujua hata kidogo, ya kwamba chini ya yadi mia moja kutoka kwake, alisimama Amiri yuyo huyo wa jeshi la Bwana, akienda Zake.

83 Ni wakati tunapowazia juu ya Mungu, tunapoanza kuota ndoto za kuwa wazima, tunapoota ndoto za kuokolewa, tunapoanza kufikiria juu ya dhambi zetu na jinsi zilivyo katili mbele za Mungu, hapo ndipo Yeye anapokaribia. Hapo ndipo wanafunzi hawa, waliovunjika mioyo, wakienda zao Emau, ambapo Yesu alitoka kwenye kile kichaka na kuanza kuzungumza nao, wakati walipokuwa wakimwazia.

84 Mnaona, shida leo hii, tuna pesa nyingi sana na kadhalika akilini mwetu, Mungu hawezi kuwa na mahali pa kuingia mawazoni mwetu. Tunataka kwenda katikati ya mji, kununua nguo mpya, ama kofia mpya, ama *kitu kingine*, halafu hatuna budi kumwona Susie na John. Tutacheza karata usiku wa leo, hatuwezi kwenda kanisani usiku wa leo, kwa sababu *Tunampenda Susie* kiko, ama kitu kama hicho, vipindi vya televisheni, tuna mengine yote niani mwetu.

85 Makanisa yana taratibu nyingi sana, na kadhalika, kutufanya tuwe na shughuli nyingi sana, mikutano ya maombi imeachwa nje. Tunahitaji kumkaribia Mungu, apate kutukaribia, enyi marafiki. Hiyo ni kweli. Lakini kila kitu kingine kimechukua mahali pa mkutano wa maombi, kila kitu kingine kimechukua mahali pa ibada halisi ya kiroho. Loo, labda dakika mbili ama tatu kanisani. Lakini ninapenda tu kujilaza na kuoga mbele Zake katika ninii Yake. . .Hivi hampendi hilo? Loo, inueni tu mikono yenu na kunywa kutoka kwenye hiyo Chemchemi, mpaka kamwe hamwezi kunywa tena, mkibubujika tu katika utamu Wake na wema Wake.

86 Nilikuwa nikizungumza na mwinjilisti mashuhuri, ndugu yangu, T. L. Osborn. Akasema, "Nilikuwa nikiwazia, Ndugu Branham, jinsi ambavyo—ambavyo kusudi langu lote ni kuokoa

nafsi, na kutoa wakati wangu wote kumwokolea Kristo nafsi," kasema, "ndipo nikawaza, vipi—vipi kuhusu upendo wangu mwenyewe na kujitolea kwangu kwa Kristo?" Kristo anampenda, pia. Anatupenda.

87 Tunaweka muda mwingi na kadhalika, bali Mungu anatutaka tuje kando, na kuketi tu chini, na kumwabudu, na kuzungumza Naye, kulizungumzia. Napenda hilo. Loo, utamu huo, huo ndio wakati mkuu kuliko zote za maisha ya mtu yeyote, ni kuketi tu chini na kutafakari, kuondoa kila kitu mawazoni mwako. Kama mngefanya hivyo, kusingekuwa na wasiwasi mwingi sana kote nchini, kama tu tungemwazia Mungu. "Nikaribieni, nami nitawakaribia."

88 Wakati ombaomba wetu kipofu ameketi pale kwenye asubuhi hiyo yenye baridi, akitetemeka, huku jua lenye joto likijaribu kuuosha mgongo wake, naye aliwazia juu ya yule Shujaa mkuu, mwenye nguvu aliyesimama moja kwa moja nje ya lango kutoka mahali alipokuwa ameketi na kuzungumza na Yoshua, akampa maagizo yote, jinsi kuta zingeanguka wakati baragumu ikipigwa, na kadhalika, alikuwa akiwazia, "Lakini huyo—huyo Mungu mkuu hawezi kufa, Yeye yu hai milele."

89 Yapata wakati huo tu akasikia kelele, Jemadari yuyo huyo mkuu, alikuwa akienda zake nje ya lango, akija Yerusalemu. Nanyi mwajua, kuna jambo fulani kulihusu, mahali Yesu alipo, kwa kawaida kuna kelele nyingi, sijui ni kwa nini, lakini hupiga kelele nyingi.

90 Mnajua kuhani mkuu, alipoingia katika Patakatifu pa patakatifu, alikuwa na. . .alitiwa manukato na mafuta ya kupaka. Na kwenye ninii yake, upindo wa vazi lake, walikuwa na komamanga na kengele, na kila wakati alipotembea, hiyo ililia, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana." Na njia pekee waliyojua alikuwa hai, wakati alipokuwa amerudi katika Patakatifu pa patakatifu, ni kwa sababu kulikuwa na kelele. Nashangaa kama hakuna mauti fulani, mahali fulani? Vema. Hiyo ndiyo njia pekee waliyojua alikuwa hai, kwa sababu alikuwa akipiga kelele huko nyuma. Walikuwa wakisikiliza waone kama kungali kulikuwa na uhai mle ndani wakati alipoingia katika Patakatifu pa patakatifu.

91 Ndipo Yesu alipotoka nje ya lango, ulikuja umati mkubwa mbio, na labda wakamkanyaga maskini, mzee ombaomba, naye alikuwa kipofu, naye akasema, "Kuna nini? Vema, kwani kuna nini?"

92 Hakuna mtu aliyemjali. Ndipo akasikia ninii, mtu fulani akisema, "Hosana, Hosana, Yeye ajaye katika Jina la Bwana! Hosana!"

93 Wanawake walikuwa wakipiga mayowe, wanaume walikuwa wakipiga mayowe, halafu angeweza kuwasikia wengine wakidhihaki na kufanya mzaha, ndipo akamsikia ki—kiongozi

wa shirika la Yerusalemu, kasisi huyo akipaza sauti, kasema, "Aisee, wewe nabii bandia, wananiambia ati ulimfufua mtu aliyekufa. Tuna uwanja mzima wa makaburi uliojaa hao hapa juu, njoo ukawafufue hawa, hebu tukuone ukiwafufua."

94 Lakini mnaona, Yesu kamwe hakuwajali pepo, aliwaacha tu waendelee. Alikuwa . . . Yeye alimjali Baba, yale, Yeye alifanya yale Baba aliyomwonyesha kufanya. Hakugeuza mawe yoyote yawe mkate. Waliweka kitambaa usoni Mwake wakati mmoja na kumpiga kichwani, kasema, "Sasa kama wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga, tutakuamini kama . . . " Wakaweka kitambaa . . . Wala kamwe Yeye hakufungua kinywa Chake na kusema neno.

95 Akining'inia msalabani, wakasema, "Ng'oa mikono yako, shuka msalabani, kama wewe ndiwe Kristo."

96 Angeweza kufanya hivyo, hakika angeweza. Angeweza kufanya hivyo, lakini kama angalifanya hivyo, angekuwa akimjali ibilisi. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, kama Billy Sunday alivyosema wakati mmoja, alisema, "Kila mti ulikuwa umekaliwa na Malaika hamsini, kasema, 'Ng'o—ng'oa tu mkono wako uuelekeze kwetu, nasi tutabadilisha mandhari hii hapa katika dakika chache.'"

97 Kayafa alisema, "Aliwaokoa wengine, mwenyewe hawezi kujiokoa," bila kujua alikuwa akimpa sifa kuu kuliko zote alizowahi kuwa nazo. Kama angalijiokoa Mwenyewe, asingeweza kuwaokoa wengine, kwa hiyo alijitoa Mwenyewe apate kuwaokoa wengine. Nina furaha kwamba Yeye aliweza kupinga majaribu ya ibilisi.

98 Yesu . . . Unaposikia watu wakisema, "Hebu nimwone akimponya *huyu*, hebu nimwone akimponya *yule*," ujue tu huyo ni ibilisi, hiyo ni sauti ile ile. Mnaona?

99 "Kuna mzee mmoja hapa chini pembeni, ana . . . anauza penseli, najua yeye ni maskini jamaa mzuri, shuka uende ukamponye. Hebu niwaone waponyaji wenu wa kiungu wakifanya hivyo." Kumbukeni tu, hiyo ni sauti ya ibilisi, hiyo ni kweli, kumbukeni tu. Hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo. Na kuna wengi wao walio namna hiyo, lakini bila shaka, pepo hawafi. I—ibilisi humchukua mtu wake, bali kamwe si roho yake; Mungu humchukua mtu Wake, bali kamwe si Roho Wake, vita vinaendelea vivyo hivyo.

100 Ndipo basi, umati huu ukakimbia, wakatoka nje na kumpigia makelele, na *hili*, *lile*. Ndipo hatimaye akasema, "Ni nini kinachoendelea? Kuna shida gani? Kuna shida gani hapa? Haraka hii yote ni ya nini? Kelele hizi zote ni za nini?" Hakuna mtu aliyekuwa akimjali.

101 Nami ninaamini, hebu tuwazie ilikuwa ni maskini mwaminio mzuri wa Bwana Yesu, labda maskini mama mmoja aliyeshuka, "Maskini jamaa huyo mzee!" Nanyi mwajua, watu wanaomfuata

Yesu, huwahurumia watu kama hao, wafuasi wa Kristo. Akashuka chini, akamwinua maskini huyo jamaa, na kusema, “Bwana, wamekusukuma kutoka kwenye hili jiwe, hapa?”

“Naam, bibiye. Nini kinaendelea?”

“Loo, hivi huelewi?”

“La.”

“Vema, uliwahi kusikia habari za Yesu wa Nazareti?”

“Siamini niliwahi kusikia,” alisema Bartimayo.

102 “Vema, Yesu wa Nazareti ndiye yule Nabii mkuu ambaye Musa alisema angeinuliwa miongoni mwa watu wetu wenyewe, anapita. Loo, kama ungaliweza kumwona Yeye, nina hakika Yeye angekufungua macho.”

“Loo, Yeye yuko wapi.”

“Loo, Yeye yuko yapata yadi mia moja ama mbili barabarani.”

Akasimama, “Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu! Unirehemu!”

103 Baadhi yao wakasema, “Loo, nyamaza! Unapiga kelele sana unanipa maumivu ya kichwa. Hao wengine hapa wakipiga makelele, pia. Nyamaza!”

“Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!”

104 Siamini Yeye angaliweza kuisikia sauti yake, kulikuwa na makelele mengi sana na kuendelea. Lakini alijua ya kwamba kama Yeye alikuwa ni yule Nabii wa Mungu, angeweza kuguswa. Ninaamini, labda alishuka kisiri, na kusema, “Ee Bwana Mungu, naomba umsimamishe. Tafadhali Bwana, unirehemu, wakati rehema inapopita.” Ndipo Yesu akasimama, akaangalia nyuma.

105 Ninaamini hilo. Yule mwanamke alipogusa vazi Lake, Yeye alihisi nguvu zikimtoka. Huyo ni Yesu yeye yule, siku chache tu baadaye. Ninii Yake, si makelele ya—yake yaliyomsimamisha, bali imani yake ilimsimamisha, nayo Biblia ilisema, “Yesu akasimama kimya.” Loo, ndugu, wakati imani ya ombaomba kipofu inaweza kumsimamisha njiani Mwake! Mtu aliyekuwa ameketi nje ya lango, ametengwa na—na, kile tungesema, jamii, naye alikuwa ni ombaomba na maskini na amevaa matambara, kipofu, na mwenye mashaka, bali imani yake ilimsimamisha Mwana wa Mungu.

106 Ni kitu gani kilichokuwa juu ya Mwana wa Mungu? Alikuwa akienda Zake Yerusalemu kusulubiwa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Uzito wote wa kila dhambi iliyopata kutendwa ulimwenguni, uliwekwa juu ya mabega Yake ya thamani. Kichwa chake kilikuwa hewani, alikuwa akitupiwa matunda na mboga zilizooza. “Mwondoeni mtu kama huyo!”

Wengine wakipaza sauti, “Hosana, Hosana!”

Huyo mwingine akapaza sauti, "Njoo, uwafufue wafu. Tuonyeshe jambo unaloweza kufanya."

107 Mchafuko kama huo, bali aliuelekeza uso Wake Yerusalemu, alijua alikuwa anaenda kule kuwafia hao watu waliokuwa wakiililia Damu Yake.

108 Ungeweza kuwazia hiyo ilikuwa ni nini? Watoto Wake Mwenyewe wakiililia Damu ya Baba. Hiyo ni kweli kabisa. Halafu basi, akiwa na hayo yote mabegani Mwake, huku yote hayo yakimkabili, huku akijua alikuja kufanya hivyo, hata hivyo, kilio na maombi na imani ya maskini ombaomba huyo mmoja kipofu bado yalimsimamisha njiani Mwake, ndipo akageuka, na kusema, "Imani yako imekuokoa." Loo, jamani! "Imani yako imekuokoa."

109 Ninaweza kuwasikia baadhi yao wakisema, "Jipe moyo. Jipe moyo."

110 Anaendelea kushuka barabarani.

111 Anasimama, akasema, "Aliniambia nini? Alisema nini sasa? 'Imani yako imekuokoa.'" Akiwa amesimama, akiangalia, baada ya kitambo kidogo, akaanza kuona vidole vyake, jambo fulani lilikuwa likitukia, imani yake ilikuwa ikithibitishwa.

112 Imani yako inaweza kumsimamisha usiku wa leo. Katika hiyo mbio kuu, kule Kuja kwa Bwana Yesu, na yote yaliyopo, hakuna mtu humu ndani aliye maskini kupindukia, ama amechakaa kupindukia, ama asiye na maana kupita kiasi, wewe si duni sana katika maadili ya maisha, usiweze kumsimamisha moja kwa moja mahali alipo sasa, Naye atasimama na kukuita *wewe*.

113 Siku moja nilisoma somo dogo juu ya Bartimayo lililosema kwamba alikuwa kipofu kwa miaka mingi, alikuwa na mke na msichana mdogo. Usiku mmoja, mke wake alikuwa mgonjwa sana, naye aka—akatoka akaenda kuomba, akasema, "Bwana, mponye mke wangu. Na endapo utamjalia mke wangu kupona . . ."

114 Ilimbidi . . . Ilikubidi kufanya jambo fulani kuufanyia umma vitimbi kidogo, la sivyo kamwe usingeweza kuwasimamisha. Kama vile huko India, na Ndugu Osborn, kama uko hapa usiku wa leo, unaelewa ninalomaanisha, wana tumbili mdogo, ama *kitu kingine* wanachopaswa kumfanyia, ama kuwa na nyo—nyoka wa swila, ama namna fulani ya kitu fulani, vitimbi kuwasimamisha watalii kupata pesa wanapopita.

115 Basi walisema Bartimayo alikuwa na njiwa wawili wadogo, nao walirukiana, na hilo lingevutia usikivu wa wa—wapita njia, watalii, na watu wanaoingia, kutoka nje ya mji.

116 Akasema, "Bwana, nampenda mke wangu, kama utamjalia kupona, kesho nitakutolea hao njiwa wawili dhabihu." Vema, mke wake akapona, naye akawapeleka hao njiwa kama dhabihu.

117 Halafu baadaye, msichana wake mdogo ambaye hakuwa amemwona maishani mwake, alikuwa amezaliwa tangu yeye alipokuwa kipofu, yapata umri wa miaka kumi na miwili, kasema alikuwa na nywele nzuri sana, za dhahabu, ni hadithi ndogo, bila shaka, basi kasema ya kwamba aliugua usiku mmoja. Naye daktari alikuwa huko, na kasema, "Bartimayo, ana homa, hawezi kabisa kuishi na homa ya namna hii."

118 Basi baada ya daktari kuondoka, alipapasa-papasa akatoka nje ya nyumba, wakati upepo ulipokuwa ukivuma karibu na kichaka cha waridi, naye akaangalia mahali alipowazia Mungu angekuwa, ndipo akasema, "Baba, sina chochote, nina kitu kimoja kilichosalia, na hicho ni mwana-kondoo wangu."

119 Na siku hizi, mmeona, ninasahau jinsi wanavyoiita wakati mbwa anapomwongoza kipofu, na kipofu, humwongoza kipofu, mbwa kipofu humwongoza kipofu, ama, mbwa humwongoza kipofu. Katika siku hizo walikuwa na mwana-kondoo aliyemwongoza kipofu badala ya mbwa, walimfundisha mwana-kondoo.

120 Bartimayo alikuwa na mwana-kondoo, naye alimwongoza akampleka mahali pake ambapo aliombea. Basi akasema, "Bwana, kama utamjalia tu msichana wangu mdogo apone, nitamchukua mwana-kondoo wangu, nami nitakutolea dhabihu."

121 Ndipo huyo msichana mdogo akapona, na kesho yake alikuwa anaenda zake kumpeleka mwana-kondoo kanisani kwenye jengo la kutolea dhabihu. Naye kuhani alikuwa amesimama kwenye, juu ya ngome za hilo jengo, akasema, "Unaenda wapi, Bartimayo kipofu?"

Akasema, "Ninaenda hekaluni kumtoa dhabihu mwana-kondoo huyu kwa Bwana."

122 "Loo," akasema, "Bartimayo kipofu, huwezi kumtoa huyo mwana-kondoo. Hapa, nitakupa thamani ya mwana-kondoo, nawe umnunue kwenye vibanda na kumtoa dhabihu."

Akasema, "Kamwe sikumwahidi Mungu mwana-kondoo *yeyote*, nilimwahidi Mwana-kondoo *huyu*."

Akasema, "Bartimayo kipofu, bali huwezi kufanya hivyo, huyo mwana-kondoo ndiye macho yako."

123 Akasema, "Kama nitatimiza neno langu kwa Mungu, Mungu atatoa Mwana-kondoo kwa ajili ya macho ya Bartimayo kipofu." Siku hii yenye baridi, ya Novemba, hivyo ndivyo Mungu alivyokuwa amefanya, alikuwa amemtoa Mwana-kondoo kwa ajili ya macho ya Bartimayo kipofu.

124 Hebu niseme jambo hili, usiku wa leo, ndugu yangu mpendwa, dada: Mwana-kondoo yuyo huyo ametolewa kwa ajili yako na kwa ajili yangu. Mungu ametoa Mwana-kondoo kwa ajili ya macho yetu ya ufahamu, kwa ajili ya ninii yetu,

Mwana-kondoo huyu alitolewa kwa ajili ya uponyaji wetu. Yeye alitolewa kusudi Roho Wake aweze kuishi miongoni mwetu kote katika siku hii, kumleta Kristo katika uhalisi kwetu, Mwana-kondoo wa Mungu ametolewa. "Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!"

Na tuombe.

125 Mungu mwenye neema, uliyejaa rehema na kweli:

> Wewe uliye Kijito cha faraja yangu yote,
> (alisema kipofu Fanny Crosby,)
> U zaidi ya maisha kwangu,
> Ni nani niliye naye duniani ila Wewe?
> Au ni nani Mbinguni ila Wewe?

Naye akapaza sauti tena:

> Usinipite, Ee Mwokozi mpole,
> Sikia kilio changu kinyenyekevu;
> Unapowazuru wengine,
> Usinipite.

126 Mpendwa Yesu, hilo ndilo ombi letu nyenyekevu, usiku wa leo. Usipite ukumbi huu hapa Tulsa usiku wa leo bila kusimama, Bwana, na kututembelea. Tunakupenda kwa mioyo yetu yote, tunakusifu kwa yote yaliyo ndani yetu. Nasi tunaamini ya kwamba Wewe ndiye Amiri jeshi mkuu yeye yule, Amiri jeshi mkuu wa wokovu wetu. Nasi tunakutazamia Wewe kuja Utukufuni siku moja, ukileta pamoja Nawe jeshi la Malaika, na kulipokea Kanisa Lako la thamani, ambao wameitwa kutoka ulimwenguni, na kuoshwa katika Damu Yako, wakibeba katika mwili wao, Jina Lako.

127 Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utatujalia, usiku wa leo, kwamba kama kuna mmoja hapa ndani, ama wengi, sijui mioyo yao, Wewe unaijua, kama hawakujui Wewe kama Mwokozi wao wa thamani, na kuhisi joto hilo la ushirika, Mungu, jalia iwe saa ii hii kwamba watakupokea na kukupenda, Nawe utasonga karibu nao. Jalia wakuwazie sasa, na wavutwe karibu. Tujalie, Bwana. Jalia kusiwe na mvulana mwenye dhambi, msichana, mwanamume, ama mwanamke, atakayetoka hapa usiku wa leo, jalia kusiwe na mtu aliyerudi nyuma atakayetoka usiku wa leo, pasipo kumjia Mungu na kusamehewa dhambi zao. Jalia walie moyoni mwao, "Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu! Nirehemu!" Tujalie, Bwana.

128 Wakati tumeinamisha vichwa vyetu na macho yetu yamefumbwa, nashangaa, katika kusanyiko hili linaloonekana usiku wa leo, ninawatakeni mwe waaminifu kabisa, na kila mtu aombe, waombee hasa wale wasiomjua Kristo sasa: Je, kuna yeyote hapa, wakati unapoomba, ungetaka tu kuinua mkono wako, hapa kwenye orofa ya chini, inua mkono wako, sio kwangu, bali Kwake, na kusema, "Ewe Mwana wa Daudi, nimekukosea, nimevunja amri Zako, unirehemu saa hii"?

Waweza kuinua mkono wako? Ili kwamba niweze tu kuwaona na kuwaombea.

129 Mungu awabariki. Mungu awabariki, kote sakafuni hapa. Huko upande wangu wa kulia, Mungu awabariki. Inua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham." Mungu awabariki. Hilo ni jema. Mungu awabariki. "Mimi huziasi sheria Zako, Ee Bwana, nataka unirehemu." Mungu ambariki mtu huyu aliyelala hapa kwenye kitanda hiki cha wagonjwa kilichowekwa hapa. Mungu na ajalie usiku wa leo kwamba unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima, bwana.

130 Huko juu kwenye roshani, upande wangu wa kulia, waweza kuinua mkono wako? Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, hilo ni jema. Mtu mwingine inua mkono wako. Nyosha tu mkono wako, huku kila jicho limefumbwa, na kila mtu akiomba; na iwe ni mimi na Roho Mtakatifu tu, tafadhali. Zile roshani za—za katikati hapa, je, kunaweza kuwako na yeyote huko juu ambaye ungeinua mkono wako? Useme, "Omba . . . "

131 Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Hilo ni jema. Roshani upande wangu wa kushoto, inua mkono wako. Mungu akubariki, mama. Mimi . . . Mungu akubariki, ewe jamaa mdogo. Huo ni msimamo mzuri sana kwa tineja, hilo ndilo jambo kuu kuliko yote ulilopata kufanya, mwanangu, huenda umefanya mambo mengi makuu, lakini hilo ndilo lililo kuu kuliko yote.

132 "Usinipite, Ee Mwokozi mpole, nataka rehema Zako sasa. Sasa kabla ya kifo changu, ninakutaka Wewe unipokee katika Ufalme Wako. Sijui hiyo itakuwa lini, huenda ikawa ni kabla ya ibada kufungwa usiku wa leo, huenda ikawa kabla sijafika nyumbani."

133 Moja ya siku hizi usiku, mahali fulani, sehemu fulani, wakati fulani mchana au usiku, utahisi mapigo ya moyo yakipanda mkononi mwako, hivyo tu basi. Loo, jamani, usiache litendeke mpaka umemjua Bwana Yesu kama mpendwa, Mwokozi wako binafsi. Kuna mwingine sasa, kabla hatujaomba? Mahali popote, mvulana, msichana, mwanamume, au mwanamke? Mungu awabariki.

134 Baba yetu wa Mbinguni, uturehemu sasa. Wa—wameinua mikono yao, wakilia, "Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!" Na jalia wao, saa ii hii, wampokee Yesu kama Mwokozi wao binafsi, jalia aje katika nguvu kuu maishani mwao.

135 Huyu kijana mwanamume hapa juu, Bwana, aliyeinua mkono wake, jambo fulani limehusika na moyo wangu kwa kilindi sana juu ya mvulana huyo. Ninaomba, Baba, labda Wewe unamwita mhudumu kwenye ibada, loo, ninaomba ya kwamba utambariki. Na hawa wengine wote walioinua mikono yao, vijana kwa wazee, jalia wampokee Yesu sasa hivi kama Mwokozi, kisha watoke hapa wakabatizwe katika kanisa fulani zuri katika imani ya Kikristo, wampokee Roho Mtakatifu, waende katika

utumishi wa Mungu kufanya lolote wawezalo kufanya kumleta Yesu katika taifa hili linalokufa na ulimwengu unaokufa. Tujalie, Baba. Utupitie usiku wa leo, Baba, ututembelee. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

136 Hebu tuimbe kifungu kimoja tu cha huo kabla hatujaendelea mbele zaidi, *Usinipite, Ee Mwokozi Mpole.*

. . . sinipite, Ee Mwokozi mpole,
Sikia kilio changu kinyenyekevu;
Unapowazuru wengine,
Usinipite.

Mwokozi, Mwokozi,
Sikia kilio changu kinyenyekevu;
Unapowazuru wengine,
Usinipite.

137 Kwa utamu sasa, hebu waaminio wote tuinue mikono yetu huku tukiuimba kwa utulivu sana.

Mwokozi, . . .

Roho ya kuabudu sasa, ujumbe umekwisha, hebu tumwabudu Bwana.

Sikia kilio changu kinyenyekevu;
Unapowazuru wengine,
Loo, usinipite.

138 Hebu tuuvumishe tu. Macho yako yamefumbwa, ukiomba tu.

139 Loo, hivi hamumpendi? Niambie jambo kuu kuliko upendo? Mungu ni upendo. Hakuna mtu atakayeweza kuonyesha jinsi Mungu alivyo upendo kama huo. Yeye ni upendo wa Agapao, upendo mkuu kuliko zote.

140 Sasa, nilikuwa tu niende kuhubiri na kufanya wito wa madhabahuni usiku wa leo, ndipo nikafika hapa, nilikuwa nimegeuzwa kabisa, nikakutana na Billy, nikasema, "Je, uligawa kadi zozote za maombi?"

141 Kasema, "La. Kamwe sikugawa kadi zozote za maombi." Lakini hatuhitaji kadi zozote za maombi kwa ajili ya ibada ya uponyaji.

142 Je, unataka . . .? Unafikiri, usiku wa leo . . .? Unampenda? Unaamini Yeye ni Bwana Yesu yeye yule? Unaamini ya kwamba imani yako ingeweza kuinuka na kusema, "Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu, mimi ni mhitaji. Ninakuhitaji, loo, ninakuhitaji; kila saa ninakuhitaji. Loo, nibariki sasa, Mwokozi wangu, naja Kwako"?

143 Unaamini ungeweza kumgusa, kumfanya ageuke, aseme, "Imani yako imekuokoa." Mnaamini mngeweza kufanya hivyo, huko nje, bila kadi za maombi? Mnaamini mna imani ya kutosha kufanya hivyo? Unaamini, inua mkono wako, useme, "Ninaamini

nina imani." Loo, hivyo ndivyo ninavyopenda kukuona ukiinua mkono wako. "Ninaamini."

144 Vema. Sijui hata mmoja wenu. Roho Mtakatifu anawajua ninyi nyote, bali Yeye yupo hapa, Uwepo Wake upo hapa, Naye angalikuwa hapa leo, angefanya tu kama alivyofanya wakati huo. Kama ulikuwa na imani ya kumgusa Yeye, Yeye angegeuka. Hivyo ndivyo ilivyofanya daima. Hiyo ilikuwa ni kweli? Imani ndiyo iliyomgusa.

145 Yule mwanamke aligusa vazi Lake, akageuka, akasema, "Ni nani aliyenigusa?" Akaangalia pande zote mpaka akamwona maskini mwanamke huyo, akasema, "Kutokwa kwako na damu kulikoma kwa sababu imani yako ilikuokoa." Mnaona? "Imani yako ilifanya hivyo." Na Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli?

146 Kama imani ya Bartimayo kipofu ingeweza kumsimamisha; kama Filipo, akisimama pale akimwangalia, angeweza kwenda kumchukua Nathanaeli, Nathanaeli angeweza kuletwa mbele Zake, Naye akamwambia mahali alipokuwa kabla hajaondoka; wakati Andrea alipoenda akamleta ndugu yake, Simoni Petro, ama, Simoni ilikuwa wakati huo, na kumleta kwa Yesu, naye Yesu alimwangalia, akasema, "Jina lako ni Simoni, baba yako alikuwa ni Yona," huyo ni Yesu yeye yule usiku wa leo. Mnaona?

147 Sasa, kuhusu kukuponya au kukuokoa, hilo tayari limefanywa. Mnaelewa hilo, sivyo? "*Alijeruhiwa* kwa makosa yetu, *alichubuliwa* kwa maovu yetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; na kwa kupigwa Kwake *tuli*," wakati uliopita . . .

148 Sasa, ninyi mlio kwenye vitanda vya wagonjwa mliolala hapa . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . watatu wao . . . [Sehemu tupu kwenye kanda.] Ninyi mlio kwenye vitanda vya wagonjwa, ninyi huko nje, ugonjwa wowote ule, chochote mnachohitaji kuombewa, mtu mwingine . . . haidhuru ni nini, Mungu anakujua . . . [Sehemu tupu kwenye kanda.] . . . na . . . ? . . . imani yako . . . [Sehemu tupu kwenye kanda.]

149 . . . sasa, kama Yeye atafanya hivyo, kama atafanya hivyo, ni wangapi wenu humu jengoni watakaosema, "Bwana, nakupenda, ninaamini ya kwamba Wewe upo hapa, ninakuthamini. Hata nitafanya upya agano langu na Wewe"? Ungefanya hivyo? Sema, "Nitaninii tu, nitajifanya upya Kwako."

150 Sasa, marafiki wa thamani, mimi ni ndugu yenu; *Hili* ni Neno la Mungu. Biblia inasema ya kwamba . . . Tumekuwa tukihubiri, kwa wageni wowote hapa, tumekuwa tukihubiri juma hili na kumwona Roho Mtakatifu akifanya hivyo, Roho Mtakatifu aliahidi, kupitia Yesu Kristo, ya kwamba katika siku za mwisho angefanya jambo lilo hilo mbele ya Kanisa, kabla tu ya Kuja Kwake. Ni wangapi wamekuwa hapa juma hili, mlisikia ikifundishwa? Yesu alisema, " . . . ilivyokuwa katika siku za

Sodoma." Mnaona? Na yule Malaika hata alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwa yule mwanamke wakati alipomwuliza Ibrahimu, "Yu wapi Sara, mkeo?"

151 Naye akasema, "Hemani, nyuma Yako."

152 Naye akacheka moyoni mwake. Akasema, "Kwa nini akacheka?"

153 Yesu alisema jambo lilo hilo litatukia kabla tu ya Kuja kwa Bwana. Ni ishara ya mwisho. Tumekuwa na uponyaji. Angalieni wakati Yesu alipojitangaza Mwenyewe: Jambo la kwanza alilofanya, alibatizwa kwa Roho Mtakatifu, wakati Yohana alipombatiza. Ninii . . . Tunaona, jambo lingine aliloanza katika huduma Yake, alianza kuwaponya wagonjwa, ndipo sifa Zake zikaenea kila mahali. Hiyo ni kweli? Ndipo, wakati hilo lilipotukia, jambo la pili, Yeye alianza kuwaonyesha ishara ya Masihi, na hapo ndipo alipokataliwa. Hapo ndipo walipomsulubisha na kumpandisha juu. Sasa, hiyo ni kweli kabisa.

154 Tumefikia ubatizo wa Roho Mtakatifu, ibada za uponyaji wa Kiungu, sasa tumefikia ile ishara kuu ya kuonekana Kwake miongoni mwetu. Jinsi tunavyopaswa kuwa na furaha, wakati hatujui ni wakati gani ulimwengu utageuka kuwa majivu.

155 Hivi mnajua, ingewezekana kabla—kabla hatujaondoka kwenye jengo hili kwamba dunia hii ingeweza kulipuliwa? Kisayansi, inasema ni usiku wa manane sasa hivi, wakati wake kutukia. Wanasayansi wote na kila kitu kinatetemeka, kila mahali, na kumbukeni, Kanisa linaenda Nyumbani kabla jambo hilo halijatukia. Basi Kuja kwa Bwana kumekaribia jinsi gani? Iweni tayari, jitayarisheni, kwa kuwa hatujui ni dakika gani wala saa anayoweza kuonekana, huenda ikawa ni wakati wowote. Tunapokea ishara yetu ya mwisho kwa Kanisa, ya Kuja Kwake.

156 Ninataka kuombea leso hizi kwa muda kidogo tu, tunapoinamisha vichwa vyetu.

157 Baba wa thamani, leso hizi, labda, zinaenda kwa maskini mama fulani wa thamani, mtoto, baba, mtu anayeteseka. Tunafundishwa katika Biblia, ya kwamba walichukua kutoka kwenye mwili wa Mtakatifu Paulo leso ama nguo, pepo wachafu wakatoka ndani ya watu, magonjwa yakaponywa. Baba, tunajua ya kwamba sisi si Mtakatifu Paulo, bali tunajua ya kwamba Wewe, Wewe ungali ni Yesu; haikuwa ni Paulo.

158 Na ilisemwa wakati mmoja, ya kwamba wakati Bahari ya Shamu ilipowakatilia mbali wana wa Israeli kutoka kwenye nchi ya ahadi, kwamba Mungu aliangalia chini kupitia ile Nguzo ya Moto kwa macho yenye hasira, ndipo bahari ikaogopa, nayo ikafanyiza ukuta, ndipo Israeli wakavuka wakaenda kwenye nchi ya ahadi katika nchi kavu.

159 Sasa, Baba, leso hizi na vifurushi vidogo vitakapowekwa juu ya wagonjwa, usiangalie sana kama kupitia Nguzo ya Moto, bali angalia kupitia Damu ya Mwanao Mwenyewe, aliyetoa ahadi. Pia jalia, wakati wowote vifurushi hivi vitakapowekwa juu ya wagonjwa, ibilisi na aogope, naomba umwangalie, Bwana, naye atajua ya kwamba hiki kimetumwa kutoka mkutanoni ambapo watu waliojazwa na Roho Wako wanaomba kwa uaminifu. Na jalia awaondokee, nao waingie mahali pale pazuri na pa afya, kwa kuwa Maandiko yanasema, "Ningependa zaidi ya mambo yote mfanikiwe katika afya." Tunavituma, katika Jina la Yesu, kwa kusudi hilo. Amina.

160 Sasa iweni na kicho. Ni wangapi walio wagonjwa huko nje? Inueni mikono yenu. Popote ulipo, inua tu mkono wako, kila mahali jengoni. Sasa iweni na kicho.

161 Sasa, ni wakati wa jinsi gani, matarajio makuu! Jambo fulani halina budi kutukia, jambo fulani halina budi kutukia, ama Biblia itaonekana imekosea, nami ni mdanganyifu wa uongo, la sivyo itaonekana kuwa ni ya kweli, na imani yetu imethibitishwa. Msijali, Kristo yupo hapa. Yeye daima . . . Yeye aliahidi jambo hilo, hawezi kufanya lolote ila kutimiza ahadi Yake. Laiti ungeamini kwa moyo wako wote sasa! Iweni tu na imani, msiwe na shaka.

162 Mnaona jambo hilo? Nuru inayoangazia papa hapa, juu ya mtu huyu papa hapa? Ana shida na macho yake. Hiyo ni kweli. Ulikuwa unaomba. Mwanao ameketi karibu nawe. Unaamini Mungu anaweza kuniambia mwanao ana shida gani? Unaamini? Ni ugonjwa wa fadhaa. Hiyo ni kweli, sivyo, mwanangu? Um-hum. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Ingekufanya ujisikie vizuri zaidi? Bw. Cullum. Hiyo ni kweli. Unaiona hiyo Nuru? Sasa pokea kile unachoomba. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

163 . . . yule yule. Hapa, papa hapa mtu mmoja ameketi, akiniangalia moja kwa moja, anaugua yabisi kavu. Amekuwa na mshtuko wa moyo. Yeye ni mhudumu. Yeye hatoki katika jiji hili, hata hatoki katika jimbo hili, anatoka Kansas. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya, bwana? Rudi Coffeyville na ujisikie vizuri sana juu yake, sivyo? Jina lako ni Kasisi Midland. Rudi, uponywe, bwana. Sikujui wewe. Kama hiyo ni kweli, punga mikono yako *hivi*. Hatufahamiani. Imani yako imekuokoa, bwana.

164 Huyo hakuwa ni mimi, rafiki yangu wa thamani, huyo alikuwa ni Bwana Yesu Kristo. Yuko huko nje miongoni mwenu, mimi ni msemaji Wake tu, nikiona kwa macho yangu yale anayofanya. Laiti mngeweza kuona kile ninachoangalia sasa. Mnaona, ni wema Wake.

165 Mwanamume aliyeketi papa hapa mwishoni, namna fulani ya Tisheti au mikono, mikono mifupi, anamwombea mtu

mwingine, hata hivyo. Anamwombea mtu aliyeketi papa hapa, anaonekana kama mtu wa Kimeksiko. Una ugonjwa wa tumbo, sivyo, bwana? Hawajakwambia jinsi . . . Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Wanakuita Joe. Hawakukwambia jinsi ulivyokuwa katika hali mbaya, bwana, bali nenda ukiamini, sasa, unaweza kuwa mzima. Mwamini Mungu.

166 Nyuma katika sehemu hii, "Kama unaweza kuamini!"

167 Huyu hapa mwanamke ameketi papa hapa chini, ameketi wa pili. Alikuwa ameinamisha kichwa chake, anaomba, "Ee Bwana Mungu, jalia aniite." Hajiombei, anamwombea mumewe. Mumewe amepata kudhoofika kwa mishipa. Amekuwa akihudhuria mikutano, bali kamwe asingeweza kurudi, amelazwa kitandani. Na sasa analia akiwa amejifunika uso kwa leso, machoni pake, kwa maana maskini mumewe yuko karibu kufa kwa sababu ya kudhoofika kwa mishipa. Usiogope, dada, chukua leso hiyo unayolilia, uiweke juu yake, usitie shaka, atapona huo.

"Kama unaweza kuamini!"

168 Huyu hapa maskini mwanamke mmoja aliyeketi moja kwa moja karibu naye, ambaye ndiyo kwanza apate imani pamoja na maskini mwanamke huyo. Anaomba, pia. Shida yake: ana shida ya kichwa chake, na macho yake, na ana ugonjwa wa tumbo. Ni mwanamke mdogo, ngoja kidogo, jina lake ni Annie. Annie, simama kwa miguu yako, Yesu Kristo anakuponya.

169 Je, mnampenda Bwana Yesu? Je, mko tayari kupokea baraka Zake? Je, mnaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake, nimewaambia ukweli? Sasa nitakwaambia jambo hili: Je, mtawekeana mikono upande wa pili?

170 Ndugu wahudumu, baadhi yenu wahubiri waaminifu hapo, shukeni mje hapa chini na kuwawekea mikono watu hawa hapa, ninawatakeni hasa juu ya mwanamke huyu *hapa*.

171 Ninyi wekeaneni mikono kwenye roshani, popote mlipo. Sasa, je, Yesu . . .?

172 Mtu huyo hapo aliye na ugonjwa huo wa tezi dume, usahau, bwana, Yesu Kristo anakuponya, nenda nyumbani.

173 Umekuwa na maumivu kwenye mapafu yako, uliyeketi papo hapo nyuma karibu na hiyo nguzo. Usiwe na hofu yoyote, umekuacha, kifua kikuu. Unaweza kwenda nyumbani na uwe mzima, Kristo Yesu anakuponya.

174 Hiyo hapo, iko tu kote jengoni, kila mahali, kila mahali. Hamwezi . . .? Loo!

> Usinipite, Ee Mwokozi mpole,
> Loo, Sikia kilio changu kinyenyekevu;
> Unapozuru wengine,
> Usinipite . . .

Ombeni sasa. Wekeaneni mikono na kuomba.

Mwokozi, Mwokozi,
Sikia. . .

175 Usiwe wa kimwili, omba, omba. Weka nia yako kwa Mungu. Usimwangalie jamaa huyo mwingine, weka nia yako kwa Mungu, kila mahali.

Wakati kwa wengine Wewe. . .("Ewe Mwana
wa Daudi, unirehemu!")
Usinipite.

Ee Mwokozi, Ee Mwokozi,

176 Mwinulieni Mungu mikono yenu sasa, semeni, "Asante, Bwana Yesu."

177 Baba wa Mbinguni, sasa tunampa ibilisi changamoto na kumkemea katika Jina la Yesu Kristo, mpaka kila nguvu za maradhi, kila giza liondoke mahali hapo, na jalia waponywe sasa hivi, kupitia Jina la Yesu.

178 Mpeni sifa, enyi watu wote, Yeye hatawapita.

179 Vema, ndugu.

60-0330 Bartimayo Kipofu
Municipal Auditorium
Tulsa, Oklahoma Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org